JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI TUNDUMA

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU WATAHINIWA 694 KUFANYA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA 2025 TUNDUMA

Tunduma, Tarehe 03 MEI 2025

Mkurugenzi Halmashauri ya Mji Tunduma, Mariam Chaurembo anapenda kuutaarifu umma kuwa jumla ya **Watahiniwa 694** wa Kidato cha Sita katika Halmashauri hiyo, wanaungana na wenzao nchini kufanya **Mtihani wa Kuhitimu Kidato cha Sita mwaka 2025** ambao unafanyika kuanzia **Jumatatu tarehe 05 Mei 2025** hadi **Jumatatu tarehe 26 Mei 2025**.

Kati ya Watahiniwa hao **694**, **Wavulana** ni **390** na **Wasichana** ni **304** ambapo Watahiniwa wa Shule ni **664** (**Wavulana ni 371 na Wasichana ni 293**), Watahiniwa wa Kujitegemea ni **30** (**Wavulana ni 19 na Wasichana ni 11**) ambapo vituo vya kufanyia mitihani ni **5** (ndani ya vituo hivyo vitano, kuna vituo viwili vya watahiniwa wa kujitegemea).

Aidha, kwa niaba ya Baraza la Madiwani, Menejimenti na Watumishi wa Halmashauri ya Mji Tunduma Chaurembo anawatakia kheri Watahiniwa wote wa Kidato cha Sita mwaka 2025 katika Mtihani wao wa kumaliza elimu ya Sekondari na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu ili wafanye vema, huku akiwataka kujiepusha na tabia zozote za udanganyifu zitakazosababisha kufutiwa matokeo yao. Hivyo, amesisitiza wazingatie taratibu zote za Mtihani wa Taifa kama zilivyowekwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Benton J. Nollo

Mkuu Wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Halmashauri ya Mji Tunduma

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji, Tunduma S.L.P 73 Simu Na: 025 295 7388, Nukushi:025 295 7391, Barua Pepe:td@tundumatc.go.tz, Tovuti:www.tundumatc.go.tz

CamScanner